FUNZO LA 15

1. Ni nani pekee apeae watu wote uhai?
-Mungu.

2. Kaini na Habili walizaliwa wapi?
-Nje ya Bustani ya Edeni.

3. Je, kwa nini Kaini na Habili walizaliwa nje ya Bustani ya Edeni?
-Kwa sababu baba yao, Adamu na mama yao, Hawa, walitenda dhambi na kutokumtii Mungu.

4. Kwa sababu Mungu aliwaondoa Adamu na Hawa katika Bustani ya Edeni, watu wote walizaliwa wapi?
-Nje ya Bustani ya Edeni.

5. Kwa nini Mungu alikubali Habili na dhabihu yake?
-Kwa sababu Habili alimtii Mungu.
-Kwa sababu Habili alimtolea Mungu dhabihu ya kondoo.
-Kwa sababu Habili alikuja kwa Mungu kupitia njia ya Mungu.

6. Je, Habili alijua nini kujihusu?
-Habili alijua kuwa alizaliwa katika dhambi.
-Habili alijua kuwa dhambi yake lazima iadhibiwe kwa kifo.

7. Je, Habili alijua nini kumhusu Mungu?
-Habili alijua kuwa Mungu ni mtakatifu.
-Habili alijua kuwa Mungu huadhibu dhambi yote kwa kifo.
-Habili alijua kuwa Mungu ni Mungu pekee anayeweza



kumuokoa.
-Habili pia alimwamini Mungu atamtuma mkombozi ili amwokoe kutokana na dhambi zake.

8. Kwa nini Mungu alimkataa Kaini na dhabihu yake?
-Kwa sababu Kaini hakumtii Mungu.
-Kwa sababu Kaini hakuleta kondoo kama dhabihu.
-Kwa sababu Kaini alijaribu kumwendea Mungu kwa njia yake, wala si kwa njia ya Mungu.

9. Je, Kaini alijifikiriaje?
-Kaini hakudhani kuwa alizaliwa katika dhambi.
-Kaini hakudhani kuwa dhambi ilipaswa kuwadhibiwa na kifo.

10. Je, Kaini alifikiriaje kumhusu Mungu?
-Kaini hakudhani kuwa Mungu ni mtakatifu.
-Kaini hakudhani kuwa Mungu huadhibu dhambi zote kwa kifo.
-Kaini hakudhani kuwa Mungu pekee angemwokoa.
-Kaini hakutaka mwokozi amwokoe kutoka kwa dhambi yake.

11. Baada ya Mungu kukataa dhabihu ya Kaini, kwa nini Mungu alinena na Kaini?
-Kwa sababu alimpenda Kaini.
-Kwa sababu Mungu alitaka Kaini akiri dhambi yake.

12. Je, Kaini alimsikiliza Mungu?
-La.

13. Je, Kaini alimsikiliza nani?

-Kaini alimsikiliza Shetani.

14. Je, Kaini alifanya nini?
-Kaini alikasirika, kisha akamuua ndugu yake, Habili.

15. Je, Mungu alikiona alichokifanya Kaini?
-Ndiyo.
-Mungu anaona kila kitu na anajua kila kitu.

16. Je, Mungu aliadhibu dhambi ya Kaini?
-Ndiyo.
-Mungu huadhibu dhambi zote.
-Hakuna dhambi hata moja ambayo Mungu haadhibu.

-Tusome alichosema Kaini baada ya Mungu kumwondoa mbele yake:

Tusome Mwanzo 4:16-19 & 23

16-Kaini akatoka mbele za uso wa Bwana, akakaa katika nchi ya Nodi, mbele ya Edeni.
17-Kaini akamjua mkewe; naye akapata mimba, akamzaa Henoko; akajenga mji akauita HHenoko, kwa jina la mwanawe.
18-Henoko akamzaa Iradi, Iradi akamzaa Mehuyaeli; Mehuyaeli akamzaa Methushaeli; Methushaeli akamzaa Lameki.
19-Lameki akajitwalia wake wawili, jina la wa kwanza ni Ada, na jina la wa pili ni Sila.
23-Lameki akawaambia wake zake, Sikieni sauti yangu, Ada na Sila; Enyi wake za Lameki, sikilizeni usemi wangu;



Maana nimemwua mtu kwa kunitia jeraha; Kijana kwa kunichubua.

-Kaini alikataa kumsikiliza Mungu.
-Kaini alimsikiliza Shetani tu.

-Kizazi cha Kaini kilifuata mfano wake.

-Kizazi cha Kaini kilikataa kumsikiliza Mungu.
-Kizazi cha Kaini kilimsikiliza Shetani tu.

-Kizazi cha Kaini kilikataa kufuata njia ya Mungu.
-Kizazi cha Kaini kilifuata njia zao tu.

-Kama vile Kaini alimuua ndugu yake, Habili, mmoja wa uzao wake, Lameki, alimuua mtu.

-Kwa sababu Kaini alikataa kumsikiliza Mungu, kizazi chake kilifuata mfano wake na pia hakikumsikiliza Mungu.

-Ni muhimu kwetu sote kumsikiliza Mungu.

-Kama hatutamsikiliza Mungu, watoto wetu watafuata mfano wetu, nao pia hawatamsikiliza Mungu.

-Kaini na kizazi chake hawakumuishia Mungu.

-Je, Kaini na kizazi chake waliishia nini maisha yao?
-Waliishia anasa, pesa na mali.

-Hatufai kuishia pesa na mali.
-Pesa na mali haziwezi kutuokoa.

-Ni Mungu tu anayeweza kutuokoa.
-Ni Mungu tu anayeweza kutuokoa kutokana na nguvu za Shetani.

-Kwa sababu Kaini alimuua Habili, Mungu aliwapa Adamu na Hawa mwana mwingine.

-Adamu na Hawa wakamuita Sethi.

Tusome Mwanzo 4:25

25-Adamu akamjua mke wake tena; akazaa mwana mwanamume, akamwita jina lake Sethi; maana alisema, Mungu ameniwekea uzao mwingine mahali pa Habili; kwa sababu Kaini alimwua.

-Je, unakumbuka Adamu na Hawa walipotenda dhambi katika Bustani ya Edeni, Mungu aliahidi kumtuma mwokozi ambaye angewaokoa watu kutoka kwa nguvu za Shetani?

-Mungu alipanga kumtuma mwokozi kupitia kizazi cha Habili kwa sababu Habili alimwamini Mungu.

-Lakini Shetani alimshawishi Kaini kumuua Habili.

-Shetani alimshawishi Kaini kumuua Habili kwa sababu hakutaka Mungu atume mwokozi ili awaokoe watu kutokana na



Shetani.

-Kwa sababu Kaini alimuua Habili, je, hio ilimzuia Mungu kufanya kile alichokuwa amepanga kufanya?
-La.

-Hakuna anayeweza kumzuia Mungu kufanya kile alichopanga kufanya.

-Kwa sababu Kaini alimuua Habili, Je, Mungu alisahau ahadi yake ya kumtuma mwokozi?
-La.

-Mungu hasahau ahadi zake.

-Je, kwa nini Mungu aliwapa Adamu na Hawa mwana mwingine aitwae Sethi?

-Kwa sababu Kaini alimuua Habili, Mungu aliamua kutuma mwokozi kupitia kizazi cha Sethi.

-Mungu hakika humaliza kazi anayoanza.

-Hakuna anayeweza kumkomesha Mungu.
-Hata Shetani hawezi kumkomesha Mungu.

-Sethi alikuwa na akaoa.
-Mke wa Sethi akamzaa mwana.

-Sethi akamuita mwana wake Enoshi.

Tusome Mwanzo 4:26

26-Sethi naye akazaa mwana; akamwita jina lake Enoshi. Hapo ndipo watu walipoanza kuliitia Jina la Bwana.

-Mungu anatuambia katika Biblia yake kuwa wakati Sethi alipomzaa mwana, familia ya Sethi ilianza kumuita Mungu na kumwamini.

-Yeyote anayemuita Mungu, na kutembea katika njia za Mungu, Mungu atamkubali.

-Weusi au weupe, tajiri au maskini, wadogo au wakubwa, waume au wake.

-Yeyote anayemuita Mungu na kwenda kwa Mungu kupitia njia ya Mungu, Mungu atamkubali.

-Ijapokuwa Sethi na familia yake walimwamini Mungu, watu wengi hawakumwamini Mungu.

-Baada ya miaka mingi, Adamu akafa.

Tusome Mwanzo 5:4-5

4-Siku za Adamu baada ya kumzaa Sethi zilikuwa miaka mia nane, akazaa wana, waume na wake.
5-Siku zote za Adamu alizoishi ni miaka mia kenda na thelathini, naye akafa.



-Kwa nini Adamu alikufa?
-Kwa sababu Adamu hakumtii Mungu, na alimsikiliza Shetani.

-Hawa pia alikufa.

-Kwa nini Hawa alikufa?
-Kwa sababu Hawa pia hakumtii Mungu, na alimsikiliza Shetani.

-Hapo mwanzo, hapakuwa na kifo ulimwenguni.

-Mungu hakutaka Adamu na Hawa wafe.
-Mungu hakutaka yeyote afe.

-Kwa nini watu wote hufa?
-Kwa sababu ya dhambi zetu.

-Je, adhabu ya Mungu kwa dhambi ni nini?
-Kifo.

-Mungu sasa anatuambia katika Biblia yake hadithi ya mzaliwa mmoja wa Sethi aitwae Henoko.

Tusome Mwanzo 5:22-23

22-Henoko akaenda pamoja na Mungu baada ya kumzaa Methusela miaka mia tatu, akazaa wana, waume na wake.
23-Siku zote za Henoko ni miaka mia tatu na sitini na mitano.

-Ijapokuwa Henoko alizaliwa mwenye dhambi, yeye alimwamini Mungu na kumtii Mungu.

-Je, Henoko alijua nini kujihusu?

-Henoko alijua kuwa alikuwa mzaliwa wa Adamu na Hawa.
-Henoko alijua kuwa alizaliwa nje ya Bustani ya Edeni.

-Henoko alijua kuwa alizaliwa katika dhambi.
-Henoko alijua kuwa alizaliwa katika kifo.

-Je, Henoko alijua nini kumhusu Mungu?

-Henoko alijua kuwa Mungu ni mtakatifu.

-Henoko alijua kuwa Mungu huadhibu dhambi zote kwa kifo.
-Henoko alijua kuwa ni Mungu pekee angeweza kumuokoa.

-Henoko alijua kuwa Mungu angemtuma mwokozi kuwaokoa watu kutoka kwa Shetani.

-Henoko aliwaambia watu wengine pia wamwamini Mungu.

-Lakini watu wengi walikataa kumsikiliza Henoko.
-Lakini watu wengi walikataa kumwamini Mungu.

-Siku moja, kitu cha kushangaza kilimfanyikia Henoko.

Tusome Mwanzo 5:24



24-Henoko akaenda pamoja na Mungu, naye akatoweka, maana Mungu alimtwaa.

-Ni nini cha kushangaza kilichomfanyikia Henoko?

-Mungu alimchukuwa Henoko mbinguni kwenda kuwa na Mungu.

-Je, mbinguni inakaa vipi?

-Mbinguni ni mahali pazuri, ambapo hakuna huzuni wala machozi.

-Mbinguni ni mahali pazuri, ambapo hakuna magonjwa au kifo.

-Mbinguni ni mahali ambapo Mungu na malaika wanaishi.

-Je, wengi wenu mmekuwa Marekani?
-La.

-Hata kama wengi wenu hamjafika Marekani, Marekani iko.

-Hata kama wengi wenu hamjafika mbinguni, mbinguni pia iko.

-Mbinguni ni wapi?
-Mbinguni ni mbali, mbele ya jua, mwezi na nyota.

-Je, kwa nini Mungu alimchukuwa Henoko kwenda mbinguni?

-Je, Henoko hakuwa na dhambi?

-Ndiyo, Henoko alikuwa na dhambi.

-Henoko alikuwa uzao wa Adamu, kama vile watu wote.

-Henoko alizaliwa katika dhambi, kama vile watu wote.

-Je, kwa nini Mungu alimchukuwa Henoko kwenda mbinguni?

-Kwa sababu Henoko alimtii Mungu.
-Kwa sababu Henoko alimwendea Mungu kwa njia ya Mungu pekee.

-Kwa sababu Mungu aliwaumba watu wote, watu wote ni wa Mungu.

-Kwa sababu Mungu aliwaumba watu wote, anaweza kufanya chochote atakacho na watu wote.

-Kwa sababu Mungu alimuumba Henoko, na Henoko alimtii Mungu, Mungu alimchukuwa Henoko kwenda mbinguni.

-Henoko hakufa.

-Kabla Henoko kufa, Mungu alimchukuwa Henoko kwenda mbinguni.

-Henoko tu ndiye hakufa, Mungu alimchukuwa kwenda mbinguni.

-Jina la mwana wa Henoko ni Methusela.



Tusome Mwanzo 5:25-27

25-Methusela akaishi miaka mia na themanini na saba, akamzaa Lameki.
26-Methusela akaishi baada ya kumzaa Lameki miaka mia saba na themanini na miwili, akazaa wana, waume na wake.
27-Siku zote za Methusela ni miaka mia kenda na sitini na kenda, akafa.

-Mwana wa Henoko, Methusela, aliishi miaka mingi zaidi ya kila mtu duniani duniani.

-Methusela aliishi kuwa miaka 969.

Tusome Mwanzo 5:28-29 & 32

28-Lameki akaishi miaka mia na themanini na miwili, akazaa mwana.
29-Akamwita jina lake Nuhu, akinena, Huyu ndiye atakayetufariji kwa kazi yetu na kwa taabu ya mikono yetu katika nchi aliyoilaani Bwana.
32-Nuhu alikuwa mwenye miaka mia tano, Nuhu akawazaa Shemu, na Hamu, na Yafethi.

-Jina la mjukuu wa Methusela ni Nuhu.
-Tutasoma kuhusu Nuhu na wana wake katika fundisho linalofuata.